

TUFAHAMU BIOS MENU NA UMUHIMU WAKE KWA SOFTWARE REPAIR

PhoenixBIOS Setup Utility							
Main	Advanced	Security	Power	Boot	Exit		
CD-ROM Drive Network boot from AMD Am79C970A +Hard Drive +Removable Devices Network boot from AMD Am79C970A #2						Item Specific Help Keys used to view or configure devices: <Enter> expands or collapses devices with a + or - <Ctrl+Enter> expands all <Shift + 1> enables or disables a device. <+> and <-> moves the device up or down. <n> May move removable device between Hard Disk or Removable Disk <d> Remove a device that is not installed.	
F1	Help	↑↓	Select Item	-/+	Change Values	F9	Setup Defaults
Esc	Exit	↔	Select Menu	Enter	Select ► Sub-Menu	F10	Save and Exit

Habari Wanandugu.

Ni Jumamosi ya kwanza leo ya somo letu la laptop repair, na katika part 2 hii tutaangalia SOFTWARE Issues Tu.

Tujue Kidogo Nini Maana Ya Software Kwenye Laptop Au Computer Yoyote

Software Kwa Lugha Rahisi Ni Part Ya Computer Ambayo Huwezi Kuishika Na Mkono, Virtual Unakiona Lakini Huwezi Kukishika, Kama Vile Application, Themes, Cursor Etc

Software Ndio Inakupa Wewe Hali ya kuzungumza na computer, Kwa lugha nyingine ni USER INTERFACE.

Kwenye laptop repair practically, Software Inajumlisha, ALL Computer Apps, Operating System, BIOS, Etc.

Kwa Leo Tuangalie BIOS MENU Ambao Ni Msingi Mkubwa Wa Software Repair Na Kwa IT Professional Yoyote Hapa ndipo pa kuanzia kwenye software repair.

BIOS ni nini?

BIOS ni program iliyo na mahusiano mojamoya na laptop au computer yoyote kwa sababu ina chip iliyopo ndani ya motherboard, chip hiyo ndiyo inafanya kazi ya kuunganisha vifaa vyote vilivyopo ndani ya computer kufanya kazi kwa usahihi, kwa lugha sahihi huu ndiyo moyo wa software kwenye computer, hii ndio mwalimu mkuu wa software zote ikiwemo Operating System, Ukibonyeza Button ya kuwasha laptop anayeguswa na kutoa ruhusa ni bios na yeye ndio anaielekeza computer, Utachukua Software Wapi Either Kwenye HDD, USB Drive Au CD ROM,Etc.

BIOS Menu Ni Nini?

Ni Mpangilio Wa BIOS Katika Laptop Unaompa Ruhusa Mtumiaji Kufanya Chaguzi Mbali Mbali Kabla Ya Kufikia Katika Operating System.

Kipi Naweza Kukifanya Kwenye BIOS Menu?

1. Unaweza Kuiwekea Password Laptop Yako (Hii ni safe Zaidi kuliko ya windows)
2. Unaweza Kuangalia Taarifa Za Laptop Yako (System Info)
3. Unaweza kuamrisha laptop yako ifuate windows kutoka kwenye Nini Mfano: HDD, USB Drive Au CD ROM
4. Unaweza Kufunga Matumizi ya Kifaa Kimoja Au Vingi Kwenye Laptop Yako, mfano: Port za USB, Speaker, Touchpad, WLAN Etc
5. Unaweza Kupunguza Nguvu za matumizi ya Laptop yako kwa kutumia menu ya Multiprocessing na Virtual Technology
6. Unaweza Kuangalia Life time na Status ya battery lako
7. Kubadili saa na kujua OS Ya Kwanza Kuwekwa Kwenye Laptop Yako.
8. Etc

NITAIPATAJE BIOS MENU?

Laptop zote zina bios menu tofauti, zinafanana baadhi kwa brand name mfano: DELL Nyingi Bios Ni F2 Na HP nyingi Bios Ni F9.

List Ya Bios Ipo Hapa Chini:

Manufacturer	Type	Boot Menu key	BIOS/UEFI key
Acer		Esc, F12, F9	Del, F2
	netbook	F12	F2
Asus	desktop	F8	F9
	laptop	Esc	Delete, F2
	netbook	Esc	F2
Compaq	Esc, F9		F10
Dell	desktop	F12	F2
	laptop	F12	F2
eMachines		F12	Tab, Del
Fujitsu		F12	F2
HP	generic	Esc, F9	Esc, F10, F1
	desktop	Esc, F9	F10, ESC
	laptop	Esc	Esc
	notebook	Esc	F10
	tower	Esc	F1
Intel		F10	
Lenovo	desktop	F12, F8, F10	F1, F2
	laptop	F12	F1, F2
	netbook	F12	F2
	notebook	F12	F2
NEC		F5	F2
		F8	F1, Del
Samsung		F12, Esc	
	netbook	Esc	F2
	ultrabook	Esc, F2	F2, F10
Sony		F11, Esc, F10, assist button	F1, F2, F3, assist button
Toshiba	laptop	F12	F2, F1, Esc, F12

1. Zima laptop yako
2. Bonyeza Key Kama Zinavyoonekana Hapo Juu (Hutegemea na BRAND YAKO)
3. Bonyeza kwa kuachia achia kama unaipiga ipiga mara nyingi maana mara nyingin hapa tunaotea
4. Unabonyeza pale laptop inapowaka na kuonyesha brand name (kuwa makini sio zote zinaonyesha brand name nyingine zinakuwa kwenye FAST BOOT)
5. Kama itagoma jaribu kwa kubonyeza huku ukiwa umeishikilia Function Key (Fn).

VILIVYOPO KWENYE BIOS MENU NA MATUMIZI YAKE

Hapa hutegemea na Bios Yenye Hapo Chini Nimetumia mfano wa Phoenix But Inaweza kuwa WARD Etc So Usikariri ila vingi vinafanana.

Tutumie mfano hapo chini.

PhoenixBIOS Setup Utility											
Main		Advanced		Security		Power		Boot		Exit	
CD-ROM Drive Network boot from AMD Am79C970A +Hard Drive +Removable Devices Network boot from AMD Am79C970A #2										Item Specific Help	
										Keys used to view or configure devices: <Enter> expands or collapses devices with a + or - <Ctrl+Enter> expands all <Shift + 1> enables or disables a device. <+> and <-> moves the device up or down. <n> May move removable device between Hard Disk or Removable Disk <d> Remove a device that is not installed.	
F1	Help	↑↓	Select Item	-/+	Change Values	F9	Setup Defaults				
Esc	Exit	↔	Select Menu	Enter	Select ► Sub-Menu	F10	Save and Exit				

MAIN = Hapo utakuta sifa za laptop yako au STEM INFORMATION

Utajua Size ya RAM, HDD, Processor Na Serial Number Ya Laptop

Sio muhimu sana kwa repair technician

ADVANCED = Hapa ni muhimu kwa technician kwa maana hapa utapata Option ya Kuzima Ports, Au WLAN au Fn Key Au Speaker, Na Touchpad Hapa Utapata Menu ya Kupunguza Nguvu Ya Pc Na Processor, Na Kwa Gamers Amba Ndio Kuna Virtual Technology, Pia Hpa ndio kuna SATA MODE Ya HDD Ukibadili Hii Windows Hauwez Run Kwa Mode Tofauti na uliyoweka wakat unafanya installation.

SECURITY = Hapa utapata menu ya kufunga Password Za Laptop Yako (BIOS PASSWORD, HDD PASSWORD, ADMIN PASSWORD).

BOOT: Hapa utapata menu ya kuamrisha laptop wapi ikachukue windows wakat inawaka, hapa ni muhimu sana wakati unataka kufanya installation ya windows kwa kutumia external device kama USB FLASH, UEFI MODE NA LEGACY MODE Zinapatikana hapa.


MATATIZO YA BIOS NA UTATUZI WAKE

Kuna matatizo mengi ya laptop lakini yafuatayo ni common na nimekumbana nayo sana.

1. BIOS PASSWORD

Hili ni tatizo sana na huwa nacharge pesa nzuri kulitatua, hii ni ile password tuliyoiona pale juu ambayo inatokea kabla booting haijafanyika.

Ukiwasha PC Utaona Hivi



JINSI YA KUTATUA TATIZO HILI

Kuna njia nyingi za kutatua BIOS Hutegemea Brand na Model Ya Laptop na Skills Alizo nazo Technician

a) Kutumia Backdoor Password: hii ni common password ambazo zipo tayari kwenye bios kutoka kwa manufacture lengo la hizi ni kutumika wakat wa Emergency Ku Reset, Ili Kupata Hizi Password, Washa PC Nenda Kwenye BIOS Password Ingiza Randomly Psssword Zozote Mara 3, Then laptop itakuandikia **SYSTEM DISABLE**, Na itakupa namba Tano Copy Hizo Namba, Then Tafuta laptop nyingine nzima Nenda Kwenye Hii Site <https://bios-pw.org>. Andika Disable code zako then Utapewa List ya Password Za Kujaribu Kufanya Reset.


b) Toa CMOS Battery.

Kama unaweza kufungua na kutoa CMOS Battery basi unaweza kufanya hivyo, Then ukawasha pc Unaweza Ukaitoa.



c) **CMOS Discharge.**


Hii ni advanced kwa tech yoyote anatakiwa kuifanya lakini ni lazima kuwa makini kwa maana ukishindwa kujua PIN Out za CMOS unaweza kuiharibu motherboard, Hii Inafanywa kwa kutoa CMOS Battery na kutafuta CMOS Pin Out Kweny Board na kupigisha Short. Means Unawasha laptop then unagusanisha hizo pin kwa kutumia Tweezer, The PC Itajizima, Ukiwasha Itakuwa haina Tena Password, Mchezo Huu Tunaufanya Sana Kwa Toshiba Na ACER, Kumbuka Kila motherboard ina PIN OUT Zake, So Kuangalia Schematica Au Ku Google Hakuepukiki. Mfano wa PIN OUT Huo hapo Chini:



d) **Kufanya Short Kwenye SCL na SDA Chip.**

SCL na SDA chip inabidi uzifanyie location kwa kutumia Schematic, Pia Utafanya Kama kwenye CMOS Discharge Hapa Utaangalia PIN out,

Mfano Hapo Chini.



2. TOUCHPAD HAIFANYI KAZI, USB PORT HAZISOMI AU WLAN HAIFANYI KAZI.

Hili na nalo ni tatizo haswaa kwa laptop za TOSHIBA, Ukifanya Kutoa Tu CMOS Battery Automatic CMOS Inafanya Reset, Mwisho wa siku inazima Touchpad kwenye BIOS Menu. USB Mode Pia Huwa Unazimwa 3.0, Mwisho wa siku Port Inakuwaga Umeme (5V) Lakini USB Device Haisomi Kabisa, Au WLAN.

SULUHISHO

Nenda Kwa BIOS Menu Upande Wa Advanced Then Angalia Kama Imezimwa Washa Na Epuka Kuchomoa CMOS Battery Mara Kwa Mara.

3. USB DEVICE HAIONEKANI WAKATI WA KUINSTALL WINDOWS KWA USB

Hii pia hutokea sana, haswaa kwa hizi laptop mpya, haijawahi kufanyiwa installation ya windows

SULUHISHO

Nenda kwa Boot Menu Angalia Kama USB Boot Device Ipo Selected Au La, Then Iweke Iwe Your First Priority, Ukiwa unayafanya haya USB Flash Drive Yenye Windows Lazima Iwepo.

MATATIZO YAPO MENGI, KAMA KUNA YOYOTE MWENYE NAYO AFANYE NYONGEZA HAPO NA KARIBUNI KWA DISCUSSION.

KUMBUKA KILA WAKATI, UKIWA UNAJIFUNZA LAPTOP REPAIR MWALIMU WAKO MKUU NI INTERNET

Wasalaam.

Mtwara Smart